

Kipeperushi: 2013-22

# Mfumo wa Ikolojia katika uvuvi mdogomdogo unaoendeshwa kwenye bahari za tropiki

Co-funded by
the European Union

WorldFish

## Lengo la mpango

Usimamizi hafifu wa uvuvi umechangia katika uharibifu wa rasilmali, kukuza umaskini na ukosefu wa uhakika wa chakula duniani kote. Ili kudhibiti hali hii, mfumo wa ikolojia, unaotoa kipaumbele kwenye uendelevu na usawa katika usimamizi wa uvuvi, umebuniwa.

Mpango huu unaoendeleza mfumo wa ikolojia katika uvuvi mdogomdogo wa bahari kwenye maeneo ya tropiki, unafadhiliwa na European Union, na unaongozwa na Taasisi ya WorldFish. Mpango huu unatekelezwa kwa ushirikiano na nchi za Indonesia, Philippines, visiwa vya Solomon na Tanzania. Lengo la mpango huu ni kutumia mfumo wa ikolojia katika usimamizi wa uvuvi ili kuboresha uendeshaji na utawala wa uvuvi mdogomdogo na kuinua uwezo wake katika kuchangia kupunguza umaskin.

Malengo mahsusi ya mpango:

1. Kutathmini mfumo wa kitaasisi uliopo na kubaini fursa zilizomo katika mfumo wa ikolojia ili kuboresha usimamizi wa uvuvi mdogomdogo na shughuli nyingine zinazoambatana nazo.
2. Kuweka mikakati na mipango kazi muafaka kwa ajili ya mfumo wa ikolojia hususan kwa mazingira ya nchi zinazoendelea; na,
3. Kuimarisha uwezo wa wadau wa uvuvi katika maeneo husika pamoja na taasisi za serkali ili waweze kushirikiana pamoja katika usimamizi wa mfumo wa ikolojia.

Mkakati uliotumika katika mpango huu ni mkakati shirikishi na unazingatia haki za jinsia - vyote ambavyo ni falsafa kuu za Taasisi ya WorldFish. Hivyo, wawakilishi wa makundi ya wadau husika watashirikishwa katika shughuli za utafiti unaohusiana na uelewa wa mfumo wa ikolojia.

## Mfumo wa ikolojia katika usimamizi wa uvuvi

Mfumo wa ikolojia unalenga kusimamia uvuvi katika ujumla wake. Ulipobuniwa awali, mfumo huu wa ikolojia ulilenga kuboresha usimamizi wa aina moja ya samaki (mf: jodari pekee) kwa kuzingatia masuala mengine yanayohusiana na uvuvi wake (mf: viumbe wanaovuliwa lakini si walengwa katika uvuvi huu, makazi ya jodari n.k). Kwa sasa, mfumo wa ikolojia hauangalii tu usimamizi wa aina moja tu ya samaki, bali mfumo huu unaangalia masuala yanahusiana na uvuvi kwa ujumla wake, ikiwa ni pamoja na kuinua juhudi zilizopo katika mifumo ya kijamii k.m. usimamizi shirikishi na usimamizi wa uwiano wa maeneo ya pwani (Integrated Coastal Management–ICM).

Shirika la Chakula Duniani (FAO) linatamka kwamba *"... mfumo wa ikolojia katika uvuvi unanuia kuweka uwiano katika malengo mbalimbali ya kijamii kwa kuzingatia masuala ya viumbe hai, vitu visivyo hai na ya binadamu, ...[aidha unanuia] kutumia mfumo huu kwenye mipaka muafaka ya kiikolojia".*

Mkakati unaotumika katika mpango huu unawalenga wadau wote na masuala yote yaliyomo katika mfumo wa ikolojia ambayo yanapaswa kuwa katika usimamizi wa uvuvi. Kwa mfano, mkakati huu unazingatia matumizi yote katika uvuvi, athari zote kwa samaki, makazi na watu, pamoja na masuala ya kijamii yanayohusiana na uvuvi – k.m. - nani hushiriki na nani hufaidika. Mkakati huu unazingatia pia masuala yasiyokuwa ya uvuvi.

Kwa mfano, tukichukulia usimamizi wa uvuvi unaoendeshwa na jamii, mfumo huu wa ikolojia unaweza kupanua wigo wa usimamizi huu kwa kutambua uwepo wa wavuvi wahamaji; samaki wanaohamahama; muingiliano wa uvuvi unaoendeshwa karibu na fukwe na ule wa mbali na fukwe; muingiliano wa nchi kavu na bahari, pamoja na masuala ya maisha ya jamii zaidi ya yale yanayohusiana moja kwa moja na uvuvi. Kwa hiyo usimamizi huu mara nyingi unawahusisha wadau wa uvuvi na wale wasiokuwa wa uvuvi katika ngazi nyingi za kiutawala.


## Mazingira ya Uvuvi Tanzania

Nchini Tanzania, uvuvi mdogomdogo una nafasi muhimu katika kuchangia uhakika wa chakula na kipato, lakini uzalishaji katika uvuvi umepungua na hali ya mazingira ya samaki baharini imeathirika. Hii inatokana na kiwango kikubwa cha uvunaji wa viumbe bahari, uvuvi usioendelevu, na unaotumia mbinu haribifu pamoja na mabadiliko ya mazingira ya pwani (unaotakana na ukataji holela wa mikoko).

Ni muhimu kutambua kuwa mazingira bora ya uvuvi na maeneo ya bahari yanachangia uendelevu wa maisha, kipato, ajira pamoja na huduma nyingine zinazotokana na mfumo wa ikolojia. Kwa hiyo hatuna budi kulinda na kuimarisha vyanzo vya faida hizi zitokanazo na mazingira asilia.

Usimamizi wa uvuvi uliopo sasa nchini Tanzania unafuata mfumo shirikishi wa kutumia vikundi vya kijamii - BMU. Hata hivyo inatambulika kwamba mifumo inayosisitiza uwiano wa masuala mbalimbali yanayohusiana katika uvuvi kama mfumo wa ikolojia unaweza ukawa wa manufaa zaidi.

Wilaya ya Bagamoyo iliyopo kaskazini mwa Dar es Salaam imeteuliwa kuwa eneo la utafiti na uendelezaji wa mfumo wa usimamizi wa kiikolojia.




Ramani: Eneo la uendelezaji usimamizi kwa mpango wa ikolojia, Bagamoyo Pwani, Tanzania (TCMP)



## Shughuli kuu za Mpango

Mwaka 2012, timu ya utafiti ilifanya tathimini shirikishi iliyohusisha makundi ya wanawake na wanaume katika jamii nane za Bagamoyo pwani. Wadau katika ngazi ya wilaya na taifa pia walishirikishwa. Utafiti huu ulihusisha:

i) kutambua maeneo na mifumo ya uvuvi mdogomdogo;
ii) Kubaini fursa na changamoto katika uvuvi huo;
iii) Kuweka vipaumbele kwa ajili ya usimamizi wa uvuvi.

Masuala mengi muhimu yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na: ongezeko na uhamiaji wa watu katika eneo la Bagamoyo, kupanda kwa gharama za maisha, mabadiliko ya matumizi ya ardhi na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa ujumla, vipaumbele vinne vikuu viliainishwa: (i) upungufu wa samaki, (ii) uharibifu wa mikoko, (iii) changamoto za kiutawala na (iv) changamoto za kujikimu kwa akina mama.

Masuala haya yalichambuliwa kwa kina zaidi katika warsha ya kuainisha vipaumbele vya usimamizi katika uvuvi kwa wilaya nzima. Kutokana na vipaumbele hivyo, masuala makuu mawili yaliibuliwa kama misingi mikuu ya kukabiliana na changamoto katika usimamizi wa uvuvi (i) elimu muafaka (*mbinu za kubainisha changamoto stahili*) na (ii) kuboresha mifumo ya usimamizi katika ngazi za chini.

Haya masuala mawili muhimu yanatarajiwa kufanyiwa kazi na timu ya utafiti katika mwaka 2013. Kwanza, utafiti wa kina utaendeshwa ili kuainisha yafuatayo:

1. Mapungufu halisi na yanayodhaniwa katika mabadiliko ya kimazingira, mifumo ya sera na taasisi pamoja na haki na wajibu wa jamii katika suala zima la usimamizi wa uvuvi.
2. Mfumo wa utawala katika Serikali za mitaa pamoja na fursa zilizopo za uwezeshaji kwa ajili ya usimamizi huu.

Utafiti huu utafuatiwa na mikakati mahsusi ya utekelezaji mwaka 2014.

## Timu ya utafiti

Timu ya utafiti inawajumuisha: Profesa Yunus Mgaya na Dkt Rosemarie Mwaipopo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt Tim Daw wa Chuo Kikuu cha East Anglia (Uingereza), Profesa Kate Brown wa The Environment and Sustainability Institute (Uingereza), na Dkt Louisa Evans anayewakilisha WorldFish. Watafiti wasaidizi ni Mr. Winfried Haule (DSM), na Mr. Egidius Kamanyi wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

## Walengwa na Wadau

Timu ya utafiti itafanya kazi na jamii za Bagamoyo pwani pamoja na taasisi za uvuvi na mazingira za kitaifa na wadau wa maendeleo. Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa elimu ya kiasili ya wananchi juu ya mazingira yao inatambuliwa na kuzingatiwa, na halafu uelewa wa mazingira haya unapanuliwa na kuboreshwa. Mafunzo yatokanayo na mpango huu yatasambazwa kwa upana na tunatumaini kuwa yakatumika na wadau wengine nchini ili kuimarisha usimamizi shirikishi wa uvuvi pamoja na malengo mengine ya kisera.

Faida za muda mrefu zinatarajiwa kuwa ni kwa jamii za Bagamoyo ambao wataimarisha mamlaka yao juu ya usimamizi wa rasilmali za uvuvi, watakuwa wameongezeka ujuzi, uelewa pamoja na kuwa na uwezo wa kuiendeleza hiyo rasilmali hadi kwa vizazi vijavyo.

## Maelezo mafupi juu ya Taasisi ya WorldFish

WorldFish ni taasisi ya kimataifa ya utafiti inayonuia kupunguza umasikini na njaa kwa kuboresha uvuvi na ufugaji wa viumbe katika maji. Taasisi hii inafanya kazi katika nchi 17 duniani na ina uzoefu na utaalamu mkubwa katika sekta za uvuvi na ufugaji wa viumbe katika maji (aquaculture).

## Mawasiliano:

Kwa mawasiliano yanayohusu mpango huu, tumia anuani zifuatazo: Dkt Rosemarie Mwaipopo (ny_lila@yahoo.com) au Dkt Louisa Evans (Louisa.evans@jcu.edu.au)



*Kutumia utafiti uletao mabadiliko*

Kunukuu chapisho hili: Mwaipopo, R., Kamanyi, E., Haule, W., Mgaya, Y., Evans, L., Daw, T., Brown, K. (2013). Mfumo wa Ikolojia katika uvuvi mdogomdogo unaoendeshwa kwenye bahari za tropiki: Tanzania. WorldFish, Penang, Malaysia. Kipeperushi: 2013-22.

The project has been funded by the European Union. The project is implemented by WorldFish in partnership with the University of Dar es Salaam, University of East Anglia (UK), the Environment and Sustainability Institute (UK).

Usanifu na Mpangilio: Eight Seconds Sdn Bhd.

Imechapishwa kwenye karatasi iliyorudufiwa kwa asilimia 100%.

Picha kwa hisani ya: Mwaipopo, Kamanyi, Haule (2012).

© 2013, WorldFish. Haki zote zinatambuliwa. Chapisho hili linaweza kurudufiwa, ila ni muhimu kutambua mhariri, WorldFish.

Anuani:
WorldFish, PO Box 500 GPO,
10670 Penang, MALAYSIA
Web: www.worldfishcenter.org

Co-funded by
the European Union

WorldFish